

JAMHURI YA MUUNGANO WATANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MIKOA WA DARES SALAAM

MTIHANI WA UTAMILIFU KIDATO CHA SITA

KISWAHILI 2

Msimbo: 121/2

Muda: saa 3:00

Jumaa 7 Februari, 2025 Asubuhi

MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina jumla ya sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **nane (8)**.
2. Jibu maswali yote kutoka sehemu A na maswali matatu kutoka sehemu B, swali la tano (5) ni la lazima.
3. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
4. Andika **namba yako ya usajili** katika kila ukurasa wa karatasi zako za kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 3 zenye maandishi

SEHEMU A (Alama 40)

1. Wewe kama msanii ukiambiwa utumie sanaa kwenye fasihi utazingatia mambo gani? Kwa kutumia mifano, eleza hoja sita (6).
2. Methali hujengwa na taswira, fafanua kauli hii ukitumia hoja tano huku ukieleza maana ya taswira hizo.
3. Maendeleo ya sayansi na teknolojia yamekuwa ni chachu ya athari hasi katika maendeleo ya fasihi simulizi, thibitisha kwa mifano madhubuti. Toa hoja tano (5).
4. Bainisha mbinu za kifani zilizotumika katika shairi lifuatalo

Karudi baba mmoja, toka safari ya mbali
Kavimba yote mapaja, na kutetemeka mwili
Watoto wake wakaja, ili kumtaka hali
Wakataka na kauli, iwafae maishani.

Akatamka mgonjwa, ninaumwa kwelikweli
Hata kama nikichanjwa, haitoki homa kali
Roho naona yachinjwa, kifo kinanikabili
Semeni niseme nini, kiwafae maishani.

Yakawatoka kinywani, maneno yenye akili
Baba yetu wathamani, sisi tunataka mali
Urithi tunatamani, mali yetu ya halali
Sema iko wapi mali, itufae maishani.

Baba aliyekufani, akajibu lile swali
Ninakufa masikini, baba yenu sina hali
Neno moja lishikeni, kama mnataka mali
Kama mnataka mali, mtaipata shambani.

SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali **matatu** kutoka sehemu hii.
Swali la **tano (5)** ni la lazima

ORODHA YA VITABU USHAIRI

Kimbunga	-	Haji Gora
Mapenzi Bora	-	Shaabani Robert
Chungu Tamu	-	Theobald A. Mvungi
Fungate ya uhuru	-	Mohamed S. Khatibu

RIWAYA

Usiku utakapokwisha	-	Mbunda Msokile
Kufikirika	-	Shaabani Robert
Mfadhili	-	Husein Tuwa
Vuta N'kuvute	-	Shafi Adam Shafi

TAMTHILIYA

Kwenye Ukingo wa Thim	-	Ebrahim Hussein
Morani	-	Emmanuel Mbogo
Kivuli kinaishi	-	Said Mohamed
Nguzo mama	-	Penina Mhando

5. "Wasanii ni mafundi wazuri sana wa kusawili jazanda ili kufikisha ujumbe kwa jamii".
Tumia diwani mbili ulizosisoma kwa kutoa hoja nne kwa kila diwani kujadili kauli hii.
6. Ushairi ni msingi mzuri wenye lengo la kujenga jamii yenye mienendo inayofaa kwa vizazi vya sasa, fafania usemi huu kwa kutoa hoja nne (4) kwa kila diwani katika ya diwani mbili ulizosoma.
7. Waandishi wa riwaya wamedadavua na kuelezea kwa kina dhana ya mapenzi. Fafania madhara ya mapenzi kwa riwaya mbili (2) ulizosoma, toa hoja nne (4) kwa kila riwaya.
8. Mara nyingi wasanii wanatofautiana katika utunzi na uwasilishaji wa kazi zao, japokuwa wanakuwa na lengo la kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa, thibitisha kauli hii kwa hoja nne (4) kwa kila tamthiliya mbili ulizosoma.